SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

MAHKAMA

SALAM ZA JAJI MKUU
MHE. KHAMIS RAMADHAN ABDALLA KATIKA KILELE CHA WIKI YA SHERIA ZANZIBAR

2024

SALAMU ZA JAJI MKUU WA ZANZIBAR MHE. KHAMIS RAMADHAN ABDALLA KATIKA KILELE CHA MAADHIMISHO YA SIKU YA SHERIA ZANZIBAR KWA MWAKA 2024

TAREHE: 07 FEBRUARI 2024

PAHALA: VIWANJA VYA MAHKAMA KUU TUNGUU

- Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dkt. Hussein Ali Mwinyi;
- Jaji Mkuu wa Tanzania, Mhe. Prof Ibrahim Hamis Juma;
- Spika wa Baraza la Wawakilishi la Zanzibar, Mhe. Zubeir Ali Maulid;
- Jaji Kiongozi wa Mahkama Kuu ya Tanzania, Mhe. Mustapha Siyani;
- Mhe. Mwalimu Haruna Ali Suleiman, Waziri wa Nchi (OR), Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora pamoja na Mawaziri na Manaibu waziri mliopo;
- Wahe. Majaji wa Mahkama Kuu mliopo;
- Mhe. Mwanasheria Mkuu wa Serikali;
- Mhe. Jaji Mkuu wa Zanzibar Mstaafu;
- Mhe. Hamisi Amiri Msumi Jaji Kiongozi Mstaafu;
- Mhe. Kadhi Mkuu wa Zanzibar;
- Mhandisi Zena Ahmeid Said, Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi;

- Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Kusini na Wakuu wote wa Mikoa mliopo;
- Mhe. Mkurugenzi wa Mashitaka Zanzibar;
- Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar;
- Mhe. Mrajis wa Mahkama Kuu ya Zanzibar na Mhe. Kaimu Msajili Mkuu wa Mahkama ya Tanzania;
- Mhe. Mtendaji Mkuu wa Mahkama Zanzibar na Mhe. Mtendaji Mkuu wa Mahkama ya Tanzania;
- Wakuu wa Vikosi vyote vya Ulinzi na Usalama mliopo,
- Makatibu wakuu na Manaibu Makatibu wakuu wa Wizara mbali mbali za Serikali mliopo;
- Waheshimiwa Wakuu wa Wilaya mliopo;
- Raisi wa Chama cha Mawakili Zanzibar;
- Wakuu wote wa Taasisi za Serikali na Binafsi mliopo,
- Wahe. Naibu Warajis, Mahakimu, Makadhi, Wakurugenzi, Viongozi na wafanyakazi wote wa Mahkama mliopo;
- Viongozi wote wa Dini na Madhehebu mbali mbali mliopo;
- Wafanyakazi wote mliopo;
- Wageni waalikwa wote, Waandishi wa habari, Mabibi na Mabwana;

Itifaki imezingatiwa.

ASSALAM ALEIKUM:

1.0 Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Awali ya yote hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kutupa neema ya uhai na kutuwezesha kukutana hapa kwa ajili ya kuadhimisha kilele cha wiki ya Sheria Zanzibar tukiwa wenye furaha na afya njema.

Pili, nachukua fursa hii kwa niaba ya Watumishi wote wa Mahkama kwa namna ya pekee kukushukuru wewe Mhe. Rais kwa kukubali mualiko wetu kwa mara nyengine tena kuwa mgeni rasmi katika maadhimisho haya ya 13 ya kilele cha wiki ya Sheria Zanzibar licha ya majukumu mengi na muhimu ya kitaifa na kimataifa yanayokukabili.

Mheshmiwa, Tokea kuchaguliwa kwako kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, hujawahi kukosa kuhudhuria kwenye maadhimisho haya. Tunasema, Ahsante sana.

Sambamaba na hayo, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa Waziri wa Nchi (OR), Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora Mhe. Mwalimu Haroun Ali Suleiman kwa mashirikiano makubwa na busara zake kwa Mhimili wa Mahkama na Taasisi za Sheria za Wizara yake kwa ujumla. Tunakiri kwa udhati wa moyoni kuwa, mashirikianao hayo ya Mhe. Waziri Haroun yameisaidia sana Mahkama na Taasisi zetu za Sheria kupata mafanikio ambayo tumeyafikia. Kwa niaba ya Mahkama, Nasema, Ahsante sana Mhe. Waziri.

2.0 Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Maadhimisho ya Siku ya Sheria huashiria kumalizika kwa mapumziko ya Mahkama na kuanza kwa Mwaka mpya wa shughuli za Mahkama. Mahkama ya Zanzibar, ilianza kuadhimisha siku hii tokea mwaka 2013. Katika maadhimisho haya, Taasisi zetu za Sheria hupata fursa ya kuwajuza wananchi juu ya huduma mbali mbali zinazotolewa na Taasisi zetu pamoja na kupima utendaji kazi wetu.

Aidha, kupitia maadhimisho haya, Taasisi za Sheria, hupata fursa ya kukaa pamoja na kubaini maeneo ambayo tumefanya vyema na yaliyokua na mapungufu na hatimae kujiwekea mikakati ya kuboresha utendaji kazi kwa kipindi kijacho cha mwaka mpya wa Mahakama.

3.0 Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Kama ilivyo kawaida , maadhimisho haya yalitanguliwa na shughuli mbali mbali zikiwemo, Mazungumzo ya Jaji Mkuu na Waandishi wa habari, ziara ya Jaji Mkuu katika Vyuo vya Mafunzo vya Unguja na Pemba kwa madhumuni ya kuwaona wanafunzi na mahabusu ili kujuwa changamoto zao za kimahkama na kutafuta ufumbuzi, utoaji wa elimu kwa wananchi, mashuleni na kupitia vyombo vya habari, huduma za msaada wa kisheria kwa wananchi, Kongamano la siku ya Sheria, matembezi ya siku ya sheria yaliombatana na huduma za uchangiaji damu nakadhalika.

4.0 Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Maadhimisho haya ya Siku ya Sheria kwa mwaka huu wa 2024 yanafanywa chini ya Kauli mbiu isemayo;

'MAZINGIRA BORA YA KAZI, MAADILI, UWAZI NA UWELEDI HURAHISISHA UPATIKANAJI WA HAKI, HUVUTIA UWEKEZAJI NA UKUWAJI WA UCHUMI.'

5.0 Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Kaulimbiu hii, inaakisi na kwenda sambamba na maono na juhudi za Serikali chini ya uongozi wako za kuboresha na kuimarisha mazingira ya utendaji kazi wa mhimili wa Mahkama na Taasisi nyengine za Sheria ili kuvutia uwekezaji nchini na kukuza uchumi wa Taifa. Kwa upande wa Mahkama, tunaitafsiri kauli mbiu hii kwa kujenga na kukuza mifumo ya uwazi, uwajibikaji pamoja na maadili kwa watumishi wote na Mawakili. Aidha, tunaendelea na juhudi za kuimarisha mafunzo kwa watumishi ili kupata watumishi wenye uweledi wa hali ya juu watakaotowa huduma bora kwa wananchi.

6.0 Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Jukumu la msingi la Mahkama ni kupokea, kusikiliza na kuyatolea maamuzi mashauri yote ya Jinai na Madai. Hivyo, naomba uniruhusu nieleze kwa ufupi tu utendaji kazi wa Mahkama kwa mwaka uliopita wa 2023 ambapo ripoti kamili ya utendaji huo utakabidhiwa hivi punde.

7.0 Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Kwa mwaka uliopita wa 2023, jumla ya mashauri 11,817 yaliendeshwa na Mahkama zetu za Zanzibar ambapo kati ya mashauri hayo, mashauri ya jinai yalikuwa ni 6,944 na mashauri ya madai yalikuwa ni 4,873. Katika kipindi hicho mashauri 8,353 yalisikilizwa na kutolewa uamuzi sawa na asilimia 70.7% ambapo mashauri yanayoendelea Mahkamani ni 3,464. Mheshimiwa Mgeni rasmi, kama

nilivyotangulia kueleza, mchanganuo wote wa hali ya usikilizaji na utoaji maamuzi wa mashauri kwa Mahkama mbali mbali za Zanzibar umeelezwa kwa kina katika ripoti ya utendaji kazi.

8.0 Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Mchakato wa utoaji wa haki unahitaji pamoja na mambo mengine, uwepo wa wafanyakazi wa kutosha wa kada mbali mbali. Kwa mwaka 2023, Mahkama iliajiri wafanyakazi wanane (8) wapya ambao ni Maafisa sheria watatu (3) na Makatibu Muhtasi watano (5). Kwa mwaka huu tumeshaomba Serikalini kibali cha kuajiri watumishi 45 ambapo wafanyakazi 17 ni kwa ajili ya kujaza nafasi tupu kwa watumishi waliofariki ama kustaafu kazi (replacement) na wafanyakazi 28 ni ajira mpya. Mheshimiwa Mgeni Rasmi naomba nitumie nafasi hii kukushukuru kwa kutupatia Majaji wapya (3) watatu, tukiamini kuwa ongezeko hili la Majaji litaongeza kasi ya usikilizaji na uamuzi wa mashauri.

Kwa upande wa kuwajengea uwezo watumishi, kwa mwaka 2024 jumla ya watumishi 27 wa Mahkama walipatiwa mafunzo ya ndani na nje ya nchi katika fani mbali mbali kwa madhumuni ya kuongeza ufanisi wa kazi. Juhudi hizi za kuwajengea uwezo watumishi wa kada mbali mbali ni endelevu kwa mujibu wa Mpango Mkakati mpya ulioandaliwa.

9.0 Mheshimiwa Mgeni Rasmi

Katika kuhakikisha nidhamu ya Maafisa wa Mahkama na watumishi wengine kwa mwaka 2023, watumishi wanne (4) wa Mahkama ikijumuisha Mahakimu wawili (2), Kadhi

mmoja na Dereva mmoja walishtakiwa mbele ya Kamati ya Maadili ya Watumishi wa Mahkama na baadae Tume ya Utumishi wa Mahkama wakituhumiwa kufanya vitendo mbali mbali vya uvunjifu wa Maadili.

Aidha, kwa kipindi hicho, Mawakili wa Kujitegemea wawili (2) na Vakili mmoja walitiwa hatiani na Kamati ya Maadili na Nidhamu ya Mawakili na kupewa adhabu.

Hivyo, kupitia salamu zangu hizi, natowa wito kwa wananchi wote, Taasisi za Serikali na binafsi kuwaripoti kwenye Kamati za Maadili, Watumishi wote wa Mahkama ama Mawakili wa kujitegemea amabao watakiuka madili ya kazi zao ili wachukuliwe hatua stahiki kwa mujibu wa sheria**.**

10.0 Mheshimiwa Mgeni Rasmi

Katika kutekeleza maelekezo ya Serikali yakuimarisha utumishi na kuondoa malalamiko ya kimaslahi kwa watumishi, Mahkama kwa kushirikiana na Tume ya Utumishi ya Mahkama imetayarisha Muundo wa Utumishi (Scheme of Service) na kuuwasilsha Kamisheni ya Utumishi wa Umma kwa hatua zaidi. Tunaamini kuwa, mara tu baada ya Muundo huo kuidhinishwa na Serikali, changamoto za kimaslahi za watumishi wa Mahkama wasiokuwa Majaji, Mahakimu na Makadhi zitatatuliwa ili kuongeza ari ya utendaji wao wa kazi.

11.0 Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Kwa upande wa maboresho ya Miundombinu ya Mahkama, kwanza kabisa, napenda kuishukuru Serikali chini ya uongozi wako kwa hatua za makusudi inazoendelea kuzichukua za kuhakikisha Mahkama inapata majengo

bora na ya kisasa. Hivi sasa, harakati za ujenzi wa majengo mapya 7 (saba) ya Mahkama zikijumuisha Mahkama za Wilaya na Mikoa katika maeneo mbali mbali Unguja na Pemba zinaendelea.

12.0 Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Ufanisi katika shughuli za Mahkama na utoaji wa haki unategemea kwa kiasi kikubwa upatikanaji wa Fedha za kutosha. Kwa mwaka wa Fedha 2023/2024 Mahkama ilipangiwa kutumia jumla ya shilingi **12,911,500,000/-** kwa kazi za kawaida. Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Febuari 2024 Mahkama imepanga kutumia jumla ya shilingi **8,835,663,000/-** na hadi kufikia mwezi wa Febuari 2024 Mahkama iliingiziwa jumla ya shilingi **6,858,781,963/-** sawa na asilimia **(77.6%)**

Kwa upande wa miradi ya maendeleo Mahkama imepangiwa kutumia shilingi **27,000,000,000/-** kati ya fedha hizo **25,000,000,000/-** kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya Mahkama za Mkoa na Wilaya na **2,000,000,000/-** zilitengwa kwa ajili ya mfumo wa usimamizi wa kesi (Case Management System).

Hadi kufikia Febuari 2024 shilingi **9,028,676,525/-** zimeanza kutumika kwa ajili ya mradi wa Ujenzi na shilingi **400,000,000/-** zimeanza kutumika kwa ajili ya kazi za mifumo.

13.0 Mheshimiwa Mgeni rasmi,

Miongoni mwa maboresho ambayo yanaendelea kufanyika ni pamoja na kuimarisha mifumo ya uwajibikaji na uwazi na kuelimisha wananchi. Kazi za utoaji elimu ya sheria kwa wananchi zinaendelea . Kitengo cha Habari na Mawasiliano kimeendelea kuratibu kazi hii ambapo kwa

mwaka 2023, kupitia Televisheni ya ZBC katika kipindi maarufu cha 'IJUE MAHKAMA' kimetayarisha na kurusha hewani jumla ya vipindi arobaini na tatu (43).

Tume ya Utumishi ya Mahkama

14.0 Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Tume hii ni chombo cha juu katika usimamzi wa utumishi wa Mahkama. Tume hii imetowa mchango mkubwa katika maboresho ya Mahkama. Kwa mwaka 2023, Tume ilifanya vikao kumi na moja (11) ambapo vikao 7 vilikuwa vya kawaida na vikao vinne (4) vilikuwa vya dharura. Aidha, Tume ilifanya ziara katika Mahkama zote za Unguja na Pemba ili kujionea mazingira ya utendaji kazi pamoja na kusikiliza changamoto za wafanyakazi na kutoa muongozo wa namna wa kuzitatuwa changamotio hizo. Tume hiyo ya Utumishi wa Mahkama ilimaliza muda wake wa kisheria wa miaka mtatu (3) tarehe 30/11/2023 na tayari Tume mpya imeshachaguliwa.

Kamati ya Kanuni

15.0 Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Kwa mwaka 2023 Kamati ya Kanuni ya Mahkama iliandaa Rasimu ya Kanuni zifuatazo:

(i) **Rasimu ya Kanuni ya Maadili ya Maofisa ya Mahkama wa Mahkama** ambayo leo tuakuomba tukukabidhi. Kanuni hii itakapoanza matumizi, itasimamia kwa ukamilifu udhibiti wa nidhamu na Maadili kwa maofisa wa Mahkama wakiwepo kazini na nnje ya maeneo yao ya kazi.

(ii) **Rasimu ya Kanuni ya Malipo ya Mawakili (Advocates' Remuneration Rules)** ambayo inaweka sawa viwango vya tozo zinazotozwa na Mawakili wa kujitegemea.

(iii) **Rasimu ya Kanuni ya Madalali wa Mahkama (Court Brokers' Rules)** ambayo inaweka mfumo wa udhibiti, usimamizi na ufuatiliaji wa shughuli za Madalali wa Mahkama na;

(iv) **Rasimu ya Kanuni ya Umalizaji wa Mashauri ya Zamani (Case Backlog Rules)** ambayo pamoja na mambo mengine inatowa tafsiri ni muda gani shauri lihukuliwe kuwa ni shauri la zamani na nini kifanyike iwapo shauri litafikia kiwango cha kuitwa kuwa ni shauri la zamani.

Rasimu ya Mahkama Maalum ya Rushwa Uhujumu wa Uchumi

16.0 Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Katika hotuba yako uliyoitowa kwenye maadhimisho ya kilele cha wiki ya Sheria kwa mwaka 2022 kwenye ukumbi wa Mikutano wa Sheikh Idrisa Abdul – Wakil Kikwajuni, uliziagiza Taasisi za Sheria kuandaa mchakato wa kutayarisha **Rasimu ya Sheria ya Mahkama ya Rushwa na Uhujumu wa Uchumi Zanzibar** ili kupambana na vitendo vya Rushwa na Uhujumu wa Uchumi katika nchi yetu. Mheshimiwa, Mahkama ilichukuwa uongozi wa suala hilo (leading role) na kwa kushirikiana pamoja na Taasisi nyengine za Haki iliunda

kikosi kazi kwa ajili ya kuandaa Rasimu hiyo. Mheshimiwa, Mgeni Rasmi nina furaha kukuarifu kuwa, Rasimu hiyo tayari imeshaandaliwa na kwa sasa inasubiri taratibu nyengine za kiserikali.

Sheria mpya ya Mahkama ya Kadhi

17.0 Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Katika azma ya kutanua wigo wa haki katika Mahkama ya Kadhi na kuondoa changamoto zilizokuwemo kwenye Sheria Kongwe ya Mahkama ya Kadhi. Sheria mpya ya Mahkama ya Kadhi Nam. 8/2024 imeundwa na kutiwa saini hivi karibuni.

Sambamba na Rasimu ya sheria hiyo, kwa mwaka 2023, Mahkama ya Kadhi imeanza mchakato wa kuandaa Rasimu ya Kanuni za Mwenendo wa Mahkama ya Kadhi ambazo zitatoa mwongozo katika masuala ya uendeshaji wa mashauri, ndoa, talaka, mirathi, Atia, Hiba, Matunzo, Malezi n.k

Utayarishaji wa Mpango Mkakati Mpya wa Mahkama

18.0 Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Ili kwenda sambamba sambamba na maboresho yanayendelea, Mahkama imekamilisha kutayarisha Mpango Mkakati wa mikaka mitano (5) 2024 - 2029. Mpango huu sasa unakuwa ndio dira ya muelekeo wa Mahkama katika kipindi cha miaka mitano (5) ijayo. Mheshimiwa hivi punde tu, tutakuomba kuuzindua Mpango Mkakati huo.

Mashirikianao na Wadau

19.0 Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Katika kuijengea uwezo wa kiutendaji Mahkama imeendelea kushirikiana na Wadau mbali mbali wa ndani na nje ya nchi. Baadhi ya wadau muhimu ambao Mahkama inaendelea kushirikiana nao ni hawa wafuatao:

Benki ya Dunia

Mahkama ya Zanzibar hivi sasa ipo katika hatua za mwisho za mazungumzo na Benki ya Dunia ili kupata fedha zitakazosaidia maeneo mbali mbali ya maboresho. Hapa naomba nichukue nafasi hii kuzishukuru Wizara za Fedha za Jamuhuri ya Muungano ya Tanzania na ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Afisi ya Raisi Katiba, Sheria, Utumushi na Utawala Bora kwa michango yao katika kuendeleza mchakato huu.

Taasisi za Haki

Taasisi hizi ni pamoja na Afisi ya Mwanasheria Mkuu, Afisi ya Mkurugenzi wa Mashataka, Jeshi la Polisi, Chuo Cha Mafunzo, Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi, Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya na Chama Cha Mawakili wa Kujitegemea. Katika mwaka 2023, kwa kushirikiana na wadau hao, Mahkama ilifanya vikao vinnne (4) vya kusukuma mbele mashauri ambapo vikao vitatu vilikuwa vya Kamati ndogo chini ya uenyekiti wa Mhe. Mrajis wa Mahkama Kuu na Kikao kimoja kilikuwa ni cha Kamati Kuu chini ya uenyekiti wa Mhe. Jaji Mkuu.

Mahkama ya Tanzania

20.0 Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Katika mwaka 2023, Mahkama ya Zanzibar imeendelea kushirikiana na Mahkama ya Tanzania katika kubadilishana uzoefu, kuwajengea uwezo watumishi, miundo mbinu ya majengo na Mifumo ya uendeshaji mashauri. Kwa upande wa miundombinu ya majengo, Mahkama ya Tanzania ipo katika hatua za mwisho za kuanza ujenzi wa Kituo Jumuishi cha Utoaji Haki huko Chake Chake Pemba. Kituo hicho kitajumuisha Mahkama za Mwanzo, Wilaya, Mkoa, Mahkama Kuu na Mahkama ya Rufaa ya Tanzania.

Aidha, Mahkama ya Tanzania inaendelea kushirikiana na Mahkama ya Zanzibar katika kuboresha mfumo wa kielektroniki wa usikilizaji wa mashauri ambapo kikosi kazi kinachojumuisha wataalamu wa pande zote mbili tayari kimeanza matayarisho ya awali.

Shirika la Maendeleo la Umoja wa Mataifa (UNDP)

Shirika hili kwa mwaka 2023, imeisaidia Mahkama katika uanzishaji wa kituo cha kuhifadhi Kumbukumbu. Aidha, shirika hili limeipatia Mahkama ya Kadhi vifaa mbali mbali vya Tehama ili kufanya kazi katika mazingira rafiki na kutoa huduma bora kwa Wananchi.

Shirika la Wanawake la Umoja wa Mataifa (UN WOMEN)

Katika Mwaka 2023, Mahkama ya Zanzibar ilishirikiana na Shirika hili katika uandaaji wa muongozo wa utoaji

wa adhabu (Sentencing Guidelines) ambao kazi hiyo inaendelea na inatarajiwa kukamilika ndani ya Mwaka huu.

Taasisi ya Basel

Katika mwaka 2023, shirika hili limeisaidia Mahkama katika uandaaji wa Muongozo wa Urejeshaji Serikalini wa Mali zilizopatikana kwa njia za uhalifu (Asset Recovery Guidelines), muongozo huo unautarajiwa kuzinduliwa ndani ya mwaka huu.

Mtandao wa Watetezi wa Haki za Binaadamu Tanzania (THRDC)

Kwa mwa mwaka 2023, Mtandao huu uliwezesha Mafunzo elekezi kwa Waheshmiwa Majaji na Mahakimu ambapo mwaka 2023, ulikuwa ni mwaka wa pili kwa Mtandao huo kuwezesha mafunzo hayo**.**

Muelekeo wa Mahkama kwa mwaka 2024

21.0 Mheshmiwa Mgeni Rasmi,

Katika mwaka huu wa 2024 Mahkama inadhamiria kutilia mkazo katika mambo yafuatayo:

1. Kuboresha Mazingira ya kazi na kuhakikisha ujenzi wa majengo saba (7) ya Mahkama ulioanza mwaka uliopita unakamilika. Aidha, kwa kushirikiana na Afisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora itahakikisha kuwa, tunakamilisha mchakato wa kurekebisha maslahi kwa watumishi wa Mahkama wasiokua Majaji, Mahakimu na Makadhi.

2. Kuendeleza Mashirikiano na wadau wetu wa ndani na nje ya nchi katika utekelezaji wa majukumu.
3. Kuendelea kusimamia kwa ukamilifu nidhamu na maadili kwa watumishi wa Mahkama na Mawakili wa Kujitegemea.
4. Kuongeza kasi ya usikilizaji wa mashauri na kutolewa uamuzi.
5. Kuendelea na maboresho kwa kufanya kazi kwa uwazi na kutoa huduma bora kwa wananchi.
6. Kwa kushirikiana na Mahkama ya Tanzania, kuendeleza na kukamilisha maboresho ya mfumo wa usikilizaji wa mashauri.
7. Kukamilisha majadiliano na Benki ya Dunia na kuanza kutekeleza mradi wa "Zanzibar Judiciary Modernization Project" (Zi-JUMP)

22.0 Mheshimiwa Mgeni Rasmi,

Baada ya salamu hizo fupi, sasa kwa heshima na taadhima, naomba nikukabidhi Ripoti ya Utendaji Kazi wa Mahkama kwa mwaka 2023 pamoja na Kanuni za Kanuni ya Maadili ya Maofisa wa Mahkama sambamba na kuzinduwa

Mpango Mkakati wa Mahkama, 2024 – 2029.

Baada ya uzinduzi huo, Mheshmiwa Mgeni Rasmi kwa heshima na taadhima nakukaribisha rasmi kutoa hotuba yako pamoja na kutupa nasaha na maelekezo yako. Mhe. Mgeni Rasmi karibu sana.